

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu: 2460117  
Fax: 255 - 022 – 2460117  
e-mail: [info@psc.go.tz](mailto:info@psc.go.tz);  
[Secretary@psc.go.tz](mailto:Secretary@psc.go.tz);  
**Website:** [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
JENGO LA UBUNGO PLAZA,  
BARABARA YA MOROGORO,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

**WATUMISHI WA UMMA WATAKIWA KUFANYA KAZI KWA  
WELEDI NA NIDHAMU**

Watumishi wa Umma nchini wametakiwa kufanya kazi kwa weledi na nidhamu kwa lengo la kutoa huduma bora kwani wananchi wanahitaji kuona wafanyakazi katika Utumishi wa Umma wanafanya kazi kwa weledi, nidhamu na maadili ya hali ya juu na kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kutoa huduma bora na kuharakisha maendeleo yanayotarajiwa na Watanzania.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Jaji (mstaafu) Dkt. Steven James Bwana amesema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2018/2019.

Amesema Haki, Maslahi, Stahili, Wajibu pamoja na Majukumu ni mambo ya msingi yanayopaswa kuangaliwa na Waajiri na Wafanyakazi wote. Kutimizwa kwake kwa usahihi huchochea ari, hamasa, juhudi, bidii na moyo wa kutenda haki na kuleta ufanisi. Hivyo, ni muhimu kila mwajiri kuhakikisha kuwa watumishi walioko chini yake wanapata haki, maslahi na stahili zao zote zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria, maelekezo yoyote halali na kwa mujibu wa masharti ya ajira zao.

Dkt. Bwana amesitiza kuwa Serikali imeonyesha juhudi kubwa za kuhakikisha watumishi wote wa Umma wanafanya kazi kwa weledi na nidhamu kwa lengo la kufikisha huduma bora kwa wananchi wote. Amelitaka Baraza kushirikiana na Tume kutekeleza kazi muhimu ya kusimamia Watumishi wa Umma na Waajiri wao kwa kuhakikisha Sheria, Kanuni na Taratibu zote katika Utumishi wa Umma zinafuatwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza hilo Bw. Nyakimura Muhoji, ambae pia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, amesema Baraza pamoja na majukumu mengine lina kazi ya kupanga Mipango na kuishauri Tume kuhusu ufanisi wa kazi na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa wakati na kwa ubora unaokubalika ili kuufanya Utumishi wa Umma kuwa wa kutukuka.

**Imetolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,  
Tume ya Utumishi wa Umma,  
**DAR ES SALAAM.**  
28 Mei, 2019